**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 2 No. 2 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i2.522


# Epistemolojia ya Waafrika katika Semi Zilizoandikwa kwenye Vazi la Kanga za Waswahili

**Martina Duwe**
*Chuo Kikuu Mzumbe-Tanzania*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2024-02-26*
*Rekebishwa: 2024-03-26*
*Kubalika: 2024-05-02*
*Chapishwa: 2024-05-05*

***Maneno Muhimu***
Epistemolojia
Kanga
Semi
Waswahili

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Duwe, M. (2024). Epistemolojia ya Waafrika katika Semi Zilizoandikwa kwenye Vazi la Kanga za Waswahili. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *2*(2), 14-24.

*Copyright © 2024*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Epistemolojia ya Waafrika, wakiwamo Waswahili hubainika kupitia sanaa inayobeba mitazamo inayozingatiwa katika jamii yao. Moja kati ya mambo yanayobainisha sanaa ya Waswahili ni vazi la kanga. Kwa jumla, usanaa katika vazi hilo hudhihirika kupitia maumbo au michoro na lugha ya kiufundi ambayo hubeba semi kama vile, mafumbo, methali na misemo. Vazi la kanga huthaminiwa na hutumiwa kwa namna mbalimbali katika maisha ya Waswahili, mathalani, kufunga kiunoni, kichwani, kujifunika na kama pambo (Hanby na Bygott, 1984). Kwa jumla, semi zilizoandikwa kwenye vazi la kanga zimefafanuliwa zaidi katika muktadha wa dhamira na dhima pasipo kumakinikiwa kwa kina katika muktadha wa kiepistemolojia kulingana na kaida za Waswahili wenyewe. Makala haya yanafafanua namna semi hizo zinavyobeba na kuhifadhi maarifa ya kiepistemolojia yanayosawiri maisha halisi ya Waswahili. Vilevile, misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi imetumika kama mwegamo mkuu katika kuchunguza, kuchanganua na kuwasilisha data husika. Matokeo yanaonesha kuwa maandishi yaliyopo katika vazi la kanga yanahifadhi fasihi ya Waswahili, hususani semi ambazo hubainisha maarifa mbalimbali, yakiwemo ya kiepistemolojia. Hivyo, makala haya yanajadili baadhi ya vipengele hivyo ambavyo ni: maarifa kuhusu kuwapo kwa kani kuu, thamani ya kazi, heshima na utiifu na uvumilivu.

## Utangulizi

Maarifa mbalimbali katika maisha ya mwanadamu huegemezwa na kutolewa kwa kuzingatia kaida za jamii husika. Kwa hiyo, neno epistemolojia hurejelewa tawi mojawapo la falsafa linalojishughulisha na uchambuzi wa maarifa ya mwanadamu katika maisha yake (Mulokozi, 2017). Epistemolojia ya Waafrika, wakiwamo Waswahili hurejelea imani, tajiriba, na mawazo yao yanayojikita katika misingi ya tamaduni zao. Tamaduni hizo huzingatiwa, huheshimiwa na huenziwa kama nyenzo ya furaha, amani na ustawi wa maisha yao. Haya yanafafanuliwa vema na Etta (2019) anayeeleza kuwa ukweli wa epistemolojia ya jamii hukitwa katika misingi fulani ya tamaduni zinazowaongoza ambazo huweza kuwa tofauti na jamii nyingine. Kwa hiyo, tamaduni za Waswahili huhifadhi na kudhihirisha maarifa ya kiepistemolojia yanayowaongoza katika kuusawiri ulimwengu wao. Maarifa hayo yamefichwa katika mwavuli wa utamaduni unaosawiriwa kupitia semi hizo.

Suala kuhusu Waswahili ni akina nani limejadiliwa na wanazuoni mbalimbali. Hoja za mjadala huo zinahusishwa na masuala ya mipaka ya kimaeneo pamoja na umilisi wa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, Mulokozi (2017) anasema kwamba Waswahili ni jamii pana inayopatikana

kwa kiasi kikubwa maeneo ya Afrika Mashariki, hususani visiwani. Anaendelea kueleza kwamba maeneo ya mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki ndiko Kiswahili kilipoanza kutumiwa na wengi, hivyo, tunawachukulia watu hao kuwa ni Waswahili. Mawazo haya yanaengua jamii nyingine zinazotumia lugha ya Kiswahili ambazo haziishi mwambao mwa Pwani ya Afrika Mashariki. Senkoro (1988) na Madumulla (2009) wanadai kuwa Waswahili, licha ya kupatikana kwa wingi katika maeneo ya Afrika Mashariki, pia wameenea katika maeneo mengi ndani na nje ya Afrika Mashariki. Wanaendelea kufafanua kwamba hata waliopo nje tunawachukulia kwamba ujuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili wameupata Afrika Mashariki au kwa watu kutoka Afrika Mashariki. Hivyo, Waswahili ni watu wote wanaozungumza Kiswahili kwa kuzingatia kaida za matumizi ya lugha hiyo na sio wale tu wanaoishi katika maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia hilo, makala haya yanawachukulia Waswahili kama watu wanaopatikana ndani au nje ya Afrika Mashariki na ambao wanauishi utamaduni wa Waswahili. Kwa jumla, imani na mawazo ya Waswahili hubainika pia kupitia sanaa inayosawiri utamaduni wao. Mathalani, kupitia michoro, picha na hata maandishi yanayoandikwa katika vitu mbalimbali, ikiwamo vazi la kanga.

Kanga ni nguo iliyosheheni mapambo na maandishi maalumu ambayo wanawake huvaa kwa kujifunga kiunoni au kujitanda mabegani au kichwani (BAKITA, 2017). Vazi hili limesanifiwa kwa ubunifu wa michoro au picha na maandishi ili kuhifadhi na kuonesha imani zinazosawiri maisha yao. Kihistoria, chimbuko la vazi hili limefafanuliwa katika mitazamo mikuu miwili. Mtazamo wa kwanza unaeleza kuwa asili ya vazi la kanga ni nchi za kigeni. Vazi hili lililetwa katika mataifa ya Afrika Mashariki na wafanyabiashara wa mwanzo kutoka bara la Asia (Beck, 2001). Hivyo, watu wa Afrika Mashariki walipata ujuzi wa kutengeneza vazi hili kutoka kwa Waasia. Mtazamo wa pili unaeleza kuwa asili ya vazi la kanga ni Afrika Mashariki. Wataalamu wa mtazamo huu mathalani, Hanby na Bygott (1984) wanaeleza kwamba asili ya vazi la kanga ni Pwani ya Afrika Mashariki, hususani Zanzibar na Mombasa. Wataalamu hawa wanaendelea kufafanua kwamba kwa mara ya kwanza vazi hili lilibuniwa na wanawake kutoka Zanzibar. Walifanikiwa kuunganisha vipande vidogo vya leso hadi wakawa na vazi lenye ukubwa uliohitajika. Vazi la kwanza kuchapishwa lilikuwa la rangi nyeusi na nyeupe. Katika miaka ya 1860 vazi hili lilijulikana kwa jina la Zhamira na baadaye liliendelea kuchapishwa kwa ubunifu zaidi (BBC News, 2017). Kutokana na kukua kwa teknolojia, vazi hili huchapishwa na kutumiwa katika nchi za Afrika Mashariki na katika nchi nyingine nyingi kama Uchina na India. Hata hivyo, katika makala haya tunalichukulia vazi hili kuwa asili yake ni Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na ukweli kwamba watu kutoka maeneo ya Afrika Mashariki, hasa Wazanzibar walikuwa na ujuzi wa kutengeneza mavazi yao hata kabla ya kuingiliana na wageni hao. Hivyo, ujio wa wageni uliongeza ujuzi wa kiteknolojia uliosaidia kuongezeka kwa ufanisi wa uchapishaji wa vazi hilo.

Vazi la kanga kwa Waswahili lina thamani kubwa na hutumika kwa madhumuni mbalimbali kama vile, kujitanda, mbeleko na kujifunga vichwani. Panapokuwa na shughuli za kijamii kwa Waswahili, hususani za kiramsa na kitanzia, ni utamaduni wao kuvaa au kujitanda kanga kama ishara ya kufurahia au kuomboleza. Kwa jumla, vazi hili huakisi sanaa ya Waswahili kifani na kimaudhui. Hii ni kutokana na ubunifu unaobainika kupitia michoro, rangi zinazotumika na maandishi yanayobainisha semi mbalimbali za Waswahili (Kisombo, 2022). Kimsingi, semi hizo huwasilisha maudhui fulani kwa jamii na hubeba na kuhifadhi imani yao juu ya masuala mbalimbali ya kimaadili. Kwa hiyo, kuna uhusiano kati ya fasihi inayobainika kupitia sanaa, ikiwemo maandishi yaliyopo kwenye vazi la kanga na mitazamo ya jamii kwayo, maarifa ya kiepistemolojia huibuliwa. Hivyo basi, makala haya yanajadili namna semi za Kiswahili katika vazi la kanga zinavyobeba vipengele mbalimbali vinavyodhihirisha epistemolojia ya Waswahili katika maisha yao halisi. Semi ni utungo au kauli fupi ya kisanaa inayobeba maana, mafunzo au ujumbe fulani kwa jamii (Mulokozi, 2017).

Utanzu huu unajumuisha vipera tofauti kama methali, nahau, mafumbo, vitendawili, simo na misemo. Kwa jumla, semi zina dhima mbalimbali katika jamii kama vile, kuonya, kuburudisha, kuhifadhi na kueneza maadili ya jamii. Tanzu za semi hubainika katika maandishi ya kanga zinazovaliwa na Waswahili. Kwa hiyo, makala haya yaajadili namna semi hizo zinavyobeba maarifa ya kiepistemolojia kulingana na tamaduni za Waswahili wenyewe.

**Kiunzi cha Nadharia**

Misingi ya Sosholojia ya Kifasihi imetumika katika kuchunguza, kuchanganua na kuwasilisha matokeo yanayohusu epistemolojia ya Waafrika katika semi zilizoandikwa kwenye vazi la kanga za Waswahili. Coser (1963) anaeleza kwamba nadharia hii ilichipuka kutokana na mawazo ya mtaalamu Charles Taylor (1822-1917) na kuendelezwa zaidi na wataalamu mbalimbali, wakiwemo Hippolyte Taine (1828-1893) na George Lukacs (1885-1971). Coser anaendelea kufafanua kwamba Taine na Lukacs katika tafiti zao waligundua kwamba mambo mbalimbali ya kijamii yanahusiana na kukamilishania. Hivyo, uumbaji wa kazi za fasihi, kwa kiasi kikubwa, hutegemea namna msanii huyo anavyofungamana na maisha ya jamii husika. Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi huelezea chanzo, sababu na hali tofauti zinazochangia kuibuka kwa kazi fulani ya sanaa inayoakisi umbile la kijamii kwa kufungamana na mila, desturi na maisha ya jamii husika. Vilevile, nadharia hii hufafanua jinsi mtunzi wa kazi ya kifasihi anavyoathiriwa na imani, itikadi, tabaka lake, mazingira ya kiuchumi, na hali ya jamii anayoimulika na kuishughulikia. Kwa jumla, makala haya yamejiegemeza zaidi katika mihimili mikuu miwili ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi. Mosi, fasihi haiwezi kujitenga na jamii ambayo, kwayo imeumbwa. Kama inavyoelezwa na Narizvi (1982), fasihi imo katika maisha halisi ya jamii. Pili, kazi ya kifasihi ni taswira halisi ya kijiografia, kimazingira, kihistoria na kiutamaduni. Katika kuchunguza vipengele vinavyodhihirisha maarifa ya epistemolojia ya Waafrika katika semi zilizoandikwa kwenye vazi la kanga za Waswahili, mtafiti amezimakinikia semi hizo kama taswira ya maisha halisi ya Waswahili. Hii imesaidia kubaini mitazamo na tajiriba za Waswahili kupitia semi zilizoandikwa katika vazi la kanga linalotumika katika mazingira yao halisi.

**Methodolojia**

Mkabala wa kitaamuli umezingatiwa katika uchunguzi na uchakataji wa matokeo ya makala haya. Kothar (2004) anasema kuwa utafiti wa kitaamuli hutumia maelezo katika kuwasilisha na kujadili data za utafiti. Anaeleza zaidi kuwa matokeo ya utafiti yanayopatikana hutolewa kwa njia ya maelezo zaidi kuliko matumizi ya kihesabu au takwimu. Kwa kuzingatia hilo, data za matokeo haya zilikusanywa kutoka vazi la kanga zinazovaliwa na Waswahili, hususani, nchini Tanzania. Kanga zilizoandikwa maandishi ya kibunifu zilitafitiwa ili kubaini maarifa ya kiepistemolojia yaliyomo ndani. Hivyo, kanga saba (7) kati ya nyingi zinazodokeza maarifa ya kiepistemolojia ziliteuliwaa na kutumika kama sampuli katika mjadala huu ili kushadidia kuwapo kwa maarifa hayo katika vazi la kanga. Izingatiwe kwamba sio maandishi yote katika kanga zinazotumiwa na Waswahili yanasawiri semi zao. Maandishi mengine ni maneno ya kawaida yasiyo na ubunifu wowote wa lugha. Hivyo, uteuzi wa kanga hizi ulizingatia kuwepo kwa semi mbalimbali za Waswahili zinazosawiri mitazamo na utamaduni wa maisha yao halisi. Kwa jumla, uwasilishaji wa matokeo yaliyopatikana ulihusisha data zilizopatikana, taarifa mbalimbali za kitafiti, pamoja na Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi.

**Matokeo ya Utafiti**

Matokeo yanaonesha kuwa vazi la kanga linalotumiwa na Waswahili huhifadhi na hubainisha vipengele mbalimbali vya epistemolojia ya Waafrika kupitia semi zilizoandikwa kwenye vazi hilo. Makala haya yanajadili vipengele vinne ambavyo ni: maarifa kuhusu kuwapo kwa kani kuu, thamani ya kazi, heshima na utiifu pamoja na uvumilivu.

**Kuwapo kwa Kani Kuu**

Kani ni nguvu ya msukumo wa kitu kilicho juu ya kitu kingine (BAKITA, 2017). Mwanadamu anaamini kuwapo kwa kani kuu inayomlinda, inayomsukuma na kumwongoza katika maisha yake ya kila siku. Chuachua (2016) anadai kwamba ipo kani iliyosababisha kuwako kwa ulimwengu na vyote vilivyomo ndani yake. Kwa mujibu wa kaida za Waafrika, Mungu ndiye nguvu kuu inayosababisha kuwapo kwa yote yalipo ulimwenguni. Dhana ya Mungu hurejelea kitu chochote kinachoabudiwa na mwanadamu kwa kuamini kuwa kina uwezo wa kumsaidia au kumtimizia mahitaji yake (TUKI, 2014). Kila jamii ina amini kuwapo kwa nguvu za Mungu kulingana na kaida zinazosawiri maisha yao halisi. Effingham (2013) ameandika kwamba Waafrika humtazama Mungu katika nyakati tatu kuu na muhimu za historia ya kuwapo kwa mwanadamu ulimwenguni ambazo ni, wakati wa kuzaliwa, kuishi na kufa. Kwa hiyo, matendo ya Waswahili yanabainisha kuwapo kwa kani hiyo kulingana na tamaduni zao.

Mungu huaminiwa kwamba ni kani inayotekeleza masuala makuu matatu katika historia ya mwanadamu. Kwanza, yeye ni asili ya kuwapo kwa vitu vyote ulimwenguni, akiwamo mwanadamu. Maamuzi yake ni sahihi daima kwa wote aliowaumba. Kwa hiyo, hakuna anayeweza kupanga azaliwe katika eneo gani, azaliwe lini, azaliwe na mtu wa namna gani na kwa namna gani. Hayo yote hupangwa na Mungu mwenyewe pasipo kuingiliwa na maamuzi ya mwanadamu yeyote yule. Hivyo, Mungu huendelea kumkumbuka kila aliyemuumba kwa kuwa ni mali yake. Katika maisha ya Waswahili, imani yao imekitwa katika kumtazama Mungu kuwa yeye ndiye sababu ya kuwapo kwao ulimwenguni. Kudhihirisha imani hii, hutumia semi kama vile, *kuzaliwa ni kudra za Mungu*, *mja hana hiyari* na *Mungu hamtupi mja wak*e. Vazi la kanga limeandikwa semi hizi ili kuendelea kuhifadhi na kueneza mtazamo wao kwamba binadamu ni mali ya Mungu kwa asili yake. Tazama mfano wa picha za kanga zenye semi hizo:




*Mungu hamtupi mja wake* ni msemo unaotumika katika maisha halisi ya Waswahili. Neno "mja" hurejelea binadamu mwenye asili ya kuumbwa na Mungu na kuwekwa katika ulimwengu huu anaoutawala. BAKITA (2017) linasema mja ni mtumwa wa Mungu; yaani asili ya mwanadamu ni Mungu hivyo, ni mali yake. Semi hii inapotumika hulenga kudhihirisha uwezo wa Mungu kwa kila mwandamu aliyemuumba. Hivyo, ni dhahiri kuwa mtazamo wa Waswahili katika asili ya kuwapo kwa mwanadamu ulimwenguni mwake kupitia semi zilizoandikwa katika vazi la kanga husawiri mtazamo mpana wa Waafrika kwamba asili ya mwanadamu ni Mungu. Haya yanabainishwa zaidi na Murphy (2003) anayeeleza kwamba imani za jamii nyingi duniani, hasa Waafrika, humtazama Mungu kuwa ni sababu ya kuwapo kwa kila kiumbe ulimwenguni, akiwemo mwanadamu. Kwa

kujiegemeza katika Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi ni dhahiri kwamba ili ubaini mitazamo ya Waafrika, hususani Waswahili lazima ujue utamaduni wao, ikiwemo fasihi inayosawiri na kutumika katika mazingira yao halisi.

Pili, yeye ni mlinzi na mfanikishaji wa kila analolihitaji mwanadamu katika maisha yake ya hapa duniani. Imani hii ya Waswahili kama jamii mojawapo ya Kiafrika hubainika kupitia sanaa inayozingatiwa katika jamii zao. Mathalani, katika mazungumzo hudhihirisha imani yao kwa Mungu kupitia semi kama vile, *nalilia uzima riziki ajuaye Mungu, mpaji ni Mungu usiudhike na hali yangu, mwomba Mungu hakosi fungu lake, riziki mafungu saba kupata ni majaliwa* na *Mama nibariki Mungu anizidishie.* Semi zenye mwegamo kama huu hubainika pia katika vazi la kanga zinazovaliwa na Waswahili wenyewe. Kimsingi, semi hizo hudhihirisha kuwa, Mungu ni mfanikishaji wa masuala yote ayatendayo mwanadamu na kila anayejiegemeza kwake hufanikiwa. Hivyo, yeye ni mkuu wa yote na hakuna mwanadamu mwenye uwezo wa kulinganishwa na nguvu zake. Picha ya kanga ifuatayo inadokeza mfano wa semi zinazohifadhi imani ya jamii kuhusu uwezo wa Mungu maishani mwao.




Maandishi yasemayo *Muomba Mungu hakosi fungu lake* kama yanavyoonekana katika picha ya kanga hiyo, ni methali inayotumiwa na Waswahili. Methali hii inabainisha imani ya jamii kuwa, maishani mwao, anayeweza kuwafanikishia yote wanayoyahitaji ni Mungu pekee. Hivyo, kila mmoja anatakiwa aamini kwamba kuna nguvu kuu juu yake na akiomba atafanikiwa kwa kila jambo. Kwao, kuishi kwa kumtegemea Mungu kuna baraka nyingi zinazoonekana na zisizoonekana. Waswahili huamini kwamba Mungu humpatia kila mmoja kipaji chake kitakacholeta utofauti baina yake na wengine wanaomzunguka katika jamii husika yake. Hivyo, mtazamo huu kuhusu uwezo wa Mungu katika maisha ya walio hai hubainika pia katika vazi lao la kanga. Jambo hili linafafanuliwa zaidi na Oladipo (2004) kwamba Waafrika huamini kuwa baada ya kuzaliwa, uhai na uzima wa mwanadamu hutegemea nguvu fulani isiyodhihirika bayana. Nguvu hiyo ni Mungu mwenyewe kupitia nyenzo mbalimbali za kumfikia, wakiwemo wazee na wahenga. Yeye ndiye huruhusu kila mwanadamu kuwa na uzima pasipo upendeleo. Naye, Effingham (2013) anaeleza kwamba Mungu pekee ndiye anayeweza kumsaidia mwanadamu katika kufanikisha na kuzishinda changamoto zinazomkabili katika ulimwengu wake. Hii ni kutokana na kuamini kwamba daima yeye anakuwa pamoja na mwanadamu akimlinda na kumwongoza. Ndio sababu kwamba katika shughuli mbalimbali kama vile kilimo, biashara na ulezi mwanadamu humwomba Mungu amsaidie kulingana na utamaduni wa imani yake. Kwa kufanya hivyo, hutegemea kupokea fungu lake kutoka kwa Mungu anayemwamini.

Tatu, yeye ni sababu mojawapo ya hatima ya maisha ya mwanadamu katika dunia yake halisi. Hii ni kwa sababu yeye ndiye aliyemweka katika dunia hii na mwisho wake upo katika maamuzi yake. Yeye hupanga na kuidhinisha kwa wakati aupendao. Jambo hilo hufanyika pasipo mwanadamu huyo kufahamu wakati na mahali kitakapotokea kifo chake (Duwe, 2022). Kifo kinapotokea watu katika jamii zao hulia na kuomboleza kwa kusema semi mbalimbali zenye muegamo wa kumtazama Mungu kama msababishaji wa jambo hilo. Kwa mfano, husema, *dunia mapito, tulie na Mungu, tulimpenda lakini Mungu kampenda zaidi, na tupe faraja yako ee Mungu*. Semi hizi hudhihirisha kuwa Waswahili wanahusisha hatima ya mwanadamu na maamuzi ya Mungu ambayo hayapingwi na mwanadamu yeyote. Kwa jumla, imani kwamba Mungu ni sababu ya kutokea kwa kifo cha mwandamu hubainika pia kupitia fasihi yao, hususani semi zilizoandikwa kwenye vazi la kanga. Ufuatao ni mfano mzuri wa semi hizo:




Msemo ulioandikwa katika picha ya kanga hii unathibitisha imani ya Waswahili inayokitwa katika kumtazama Mungu kama sababu ya kifo cha mwanadamu. Hivyo, maamuzi yake juu ya jambo hilo hayapingwi na yeyote. *Tulimpenda lakini Mungu kampenda zaidi* ni msemo unaotumika wakati wa maombolezo katika mazingira halisi ya Waswahili. Mantiki inayopatikana katika msemo huu inaakisi mtazamo wao kuwa kuna nguvu inayomsukuma mwanadamu kutoendelea kuishi katika dunia hii. Nguvu hiyo ni Mungu mwenyewe. Hivyo, hata mwanadamu akipendwa namna gani na watu wanaomzunguka katika jamii yake, Mungu humpenda zaidi. Kwa hiyo, kwa wakati wake Mungu huamua kumchukua pasipo makubaliano na mwanadamu yeyote. Imani kuhusu Mungu ni sababu ya kutokea kwa kifo cha mwanadamu kupitia semi zinazoandikwa katika kanga za Waswahili huyasawiri maarifa ya kiepistemolojia ya Waafrika. Murphy (2003) anaeleza kwamba moja kati ya sababu za kifo cha mwanadamu zinazotawala zaidi fikra za Waafrika ni Mungu. Hivyo, kila kinapotokea kifo cha mwanadamu katika jamii za Kiafrika watu hutoa sababu kadhaa za kutokea kwake, miongoni mwake ikiwa ni maamuzi ya Mungu. Mtazamo kuhusu uwezo wa Mungu unaobainika katika semi zilizoandikwa kwenye vazi la kanga la Waswahili hudhihirisha imani yao. Kama wasemavyo Wanasosholojia wa Kifasihi, fasihi na maisha halisi ya jamii haviwezi kutenganishwa. Badala yake hutegemea na kukamilishana.

**Thamani ya Kazi**

Kuwajibika katika maisha ya Waafrika ni suala linalohimizwa na kuzingatiwa katika jamii yao. Maarifa ya msingi yanayosisitizwa kwa jamii ni kutambua na kuenzi uzalishaji mali kama nguzo ya uhai wa maisha binafsi, kaya, na ustawi wa jamii. Kwao, ufanywaji wa kazi huzingatia mgawanyo wa majukumu kulingana na kaida zinazozingatiwa. Kufanya kazi husababisha familia kuwa na maisha bora. Mtu asiyefanya kazi pasipo sababu yoyote, mathalani ugonjwa, katika jamii za Waafrika, wakiwemo Waswahili hukosa thamani. Hatimaye, mtu huyo hasikilizwi hasa katika kutoa maamuzi ya shughuli muhimu katika jamii yake. Haya yanaelezwa vyema na Aju na wenzake (2013) wanaodai kuwa jamii nyingi za Kiafrika humthamini mtu anayefanya kazi na kuongeza kipato kinachosaidia kuendesha maisha yake, familia na jamii. Hivyo, kazi humletea mtu heshima na akiikosa hujiona kama asiye na mchango mkubwa katika familia na jamii yake. Maishani mwao Waswahili hutumia semi mbalimbali zinazobainisha mtazamo kuhusu kazi. Mathalani, semi kama vile, *punda afe mzigo ufike, jembe halimtupi mkulima, kazi ni kipimo cha utu, mchagua jembe si mkulima, zege halilali, mwenda bure si sawa na mkaa bure na mwanamume hasifiwi kula anasifiwa kazi.* Semi zenye mwegamo huu zimehifadhiwa pia katika vazi la kanga zinazotumiwa na jamii ya Waswahili. Ufuatao ni mfano wa picha za kanga zinazoonesha semi hizo:




*Kazi ni kipimo cha Utu* ni msemo unaotumiwa na Waswahili kulingana na tamaduni zao kwa lengo la kuhimiza watu wafanye kazi ili kuwa na jamii iliyostawi na kuneemeka. Utu ni hali ya kuwa na tabia nzuri ya kibinadamu (BAKITA, 2017). Kwa hiyo, katika jamii ya Waswahili, kufanya kazi yoyote halali ni kigezo kimojawapo cha mtu huyo kuwa na utu. Hii ni kwa sababu, maishani mwao, kufanya kazi kuna tija kubwa katika ustawi wa jamii. Waswahili kama sampuli ya jamii pana ya Waafrika hutambua na kuenzi uzalishaji mali kulingana na mgao wao wa majukumu. Hivyo, huamini katika kuwajibikaji kwa moyo bila kutazama vikwazo au changamoto zilizopo mbele ili kufanikisha lengo husika. Kwao, anayewajibika katika shughuli mbalimbali za kijamii, ndiye afaaye katika ustawi na ulinzi wa amali za jamii husika. Yule anayekwenda kinyume huchukuliwa kuwa anakiuka maadili ya jamii kulingana na mgao wao wa majukumu (Oruka, 1990). Kwa hiyo, utu wa mwanadamu hubainika kupitia yale anayoyafanya ambayo yana tija katika maendeleo ya familia na jamii yake. Kwa kujiegemeza katika Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi ni ukweli usiopingika kwamba mitazamo ya Waafrika, hususani Waswahili kuhusu thamani ya uwajibikaji kupitia semi zilizoandikwa katika vazi la kanga huakisi mazingira, hali ya kiuchumi na utamaduni wa maisha yao. Kuwajibika katika

kufanya kazi, kwao, ni nguzo ya uhai na thamani ya maisha ya mwanadamu katika ngazi ya kaya, ukoo, jamii na taifa. Semi zinazoandikwa kwenye vazi la kanga zinadokeza uzingatizi wa maarifa ya uwajibikaji unaokitwa katika urithishwaji wa majukumu kwa jamii.

**Heshima na Utiifu**

Heshima na utiifu ni baadhi ya maadili yaliyojikita katika imani za Waswahili. Daima Waswahili husisitiza suala la heshima na utiifu kama silaha ya kila mwanadamu katika mazingira yake halisi. Maarifa haya huendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Heshima ni mwenendo mwema au adabu (BAKITA, 2017). Utiifu ni uzingatizi wa taratibu zilizopo bila kulazimishwa. Dhana hizi zinatofautiana kimaana lakini zinakamilishana kimantiki. Mara zote mtu mwenye utiifu katika jamii za Waswahili hutazamwa kuwa ni mwenye heshima. Kwa hiyo, si rahisi kuzitenganisha dhana hizi katika kurejelea mwenendo wa mwanadamu. Suala la utiifu katika jamii za Waswahili husisitizwa kupitia sanaa zao mbalimbali, ikiwemo fasihi yao. Hivyo, zipo semi mbalimbali zinazozungumzwa na kuandikwa katika vitu mbalimbali, ikiwemo kanga zinazodokeza maarifa kuhusu heshima na utiifu. Mathalani, *heshima hainunuliwi, utii ni silaha ya kuvuna mema, utu wa mtu ni heshima na jiheshimu uheshimiwe.* Hivyo, kila anayesoma maandishi hayo hupata funzo litakalomtafakarisha na kujihoji juu ya namna anavyowatii na kuwaheshimu wengine. Ifuatayo ni picha ya kanga inayoonesha mfano wa semi hizo:




*Utu wa mtu ni heshima na upendo* kama inavyobainika katika picha ya vazi la kanga hii ni msemo unaotumiwa na Waswahili ukihifadhi imani yao kwamba heshima ni msingi wa utu wa mtu katika ulimwengu wake. Imebainika kuwa kanga iliyoandikwa msemo kama huu inapovaliwa, wanaosoma wanapata ujumbe unaosisitiza suala la kuwaheshimu watu wote wanaomzunguka. Kwa Waswahili, mtu mtiifu na mwenye heshima huthaminiwa na huchukuliwa ni mwenye utu. Heshima, utiifu na unyenyekevu kwao, ni vipengele muhimu vinavyobainisha mtazamo wa kimaadili katika mazingira yao halisi. Naye, Agozino (2018) anadai kwamba suala la heshima, utiifu na unyenyekevu kwa Waafrika huanzia katika ngazi ya familia kisha jamii nzima. Anaendelea kueleza kwamba vitendo kama vile, kusalimia wakubwa, kuomba msamaha, kusaidia wengine kazi mbalimbali na kutumia lugha faafu kulingana na utamaduni wa jamii, ni baadhi ya mambo yanayoashiria suala la heshima na utiifu kwa Waafrika. Kila mmoja ana jukumu la kuwatii wazazi au walezi, wakubwa wote na mamlaka mbalimbali za uongozi zilizopo katika jamii kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa. Mtazamo huu husisitizwa katika maisha halisi ya Waswahili kupitia fasihi yao, zikiwemo semi zilizoandikwa kwenye vazi la kanga. Hii ni kwa sababu fasihi ni zao la jamii hivyo, huhifadhi na kubainisha

mitazamo yao kama wasemavyo Wanasosholojia wa Kifasihi kwamba kazi ya sanaa ni taswira halisi ya jamii husika.

**Uvumilivu**

Suala la uvumilivu katika maisha ya Waswahili huchukuliwa kuwa ni kigezo muhimu cha kupima utoshelevu wa imani ya mwanadamu katika kufikia azma fulani. Uvumilivu ni hali ya kustahimili machungu (TUKI, 2014). Hivyo, katika maisha ya Waswahili hutoa mafunzo mbalimbali yanayohusu faida za uvumilivu kwa vijana wao kwa kutumia fasihi, hususani semi. Kila anayesikiliza au kusoma semi zilizoandikwa katika kazi yoyote ya sanaa, ikiwemo vazi la kanga, hupata funzo ambalo litamsaidia kutafakari juu ya kufanikiwa kwa malengo yake. Waswahili huamini kwamba mtu mwenye uvumilivu katika jambo lolote analolipambania, hufanikiwa. Imani hii hurithishwa kizazi hadi kizazi kingine kupitia fasihi yao, mahususi semi mbalimbali kulingana na kaida zao. Kwa mfano, semi zisemazo, *moyo wangu tulia kila jambo ni hatua, mvumilivu hula mbivu, baada ya dhiki faraja, mchumia juani hula kivulini* na *uvumilivu ni silaha ya mafanikio*, husisitizia jamii kuwa na uvumilivu katika kila jambo. Licha ya kutumia semi hizi katika mazungumzo yao ya kila siku, vazi la kanga linalotumiwa na Waswahili wenyewe linahifadhi maarifa haya. Mfano mzuri ni semi katika picha ya kanga ifuatayo:




*Mvumilivu hula mbivu* kama inavyosomeka katika picha ya kanga hiyo ni methali inayotumiwa na Waswahili katika kutoa mafunzo kwa vijana na jamii yanayolenga kutokata tamaa katika kuliendea jambo lolote lenye tija. Hii inatokana na imani yao kuwa mafanikio yoyote ya mwanadamu huja kwa kuambatana na changamoto mbalimbali. Kwa hiyo, uvumilivu ni silaha ya kushinda changamoto na kufikia mafanikio yanayotarajaliwa. Kanga za Waswahili kuandikwa methali zenye mwegamo wa maarifa ya uvumilivu ni mbinu mojawapo inayotumiwa na Waswahili katika kufikisha mafunzo lengwa kwa jamii. Kila anayesoma maandishi hayo hupata hisia za kutiwa moyo katika magumu anayopitia katika kufikia malengo yake. Haya yanasisitizwa na Wanasosholojia wa Kifasihi kwamba kinachohifadhiwa na kubainika katika umbo la sanaa, zikiwemo semi kwenye kanga husawiri mitazamo na tajiriba ya jamii husika. Waswahili huamini kwamba uvumilivu katika jambo lolote huhitaji subira ya mtu. Subira hiyo ni katika kutoa maamuzi au kutenda jambo husika. Kwa hiyo, hutumia semi mbalimbali kuonesha kwamba jambo lolote likiendewa kwa pupa huleta athari hasi kwa mwanadamu mwenyewe, familia na (au) jamii nzima. Hivyo, tafakuri ya kina huhitajika katika kutoa maamuzi ili kuepusha athari hizo. Jambo hili husisitizwa kupitia semi mbalimbali za Kiswahili kama vile, *subira yaleta heri, kawia ufike, polepole ndio mwendo* na *mwenda pole hajikwai*. Semi kama hizi

Vol. 2 No. 2 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i2.522


hubainika pia katika vazi la kanga zinazotumiwa katika jamii zao. Maandishi katika picha ya kanga ifuatayo yanabainisha maarifa hayo:




Maandishi yasemayo *subira yaleta heri* ni semi iliyopo katika kategoria ya methali. Semi hii hutumiwa na Waswahili kwa lengo la kuhamasisha kufanya kazi na kutia moyo juu ya jambo fulani. Kusubiri jambo lolote kunahitaji muda na uvumilivu. Kipindi cha kusubiri kinaendana na tafakuri itakayomfanya mtu awe na maamuzi sahihi juu ya jambo hilo. Tafakuri hiyo huongozwa na imani fulani kuhusu kuwapo au kutokea kwa jambo hilo kwa wakati unaosubiriwa. Kijogoo (2020) anaeleza kwamba jambo lolote lenye tija katika maisha ya mwanadamu linatakiwa liendewe kwa umakini unaoambatana na subira. Subira hiyo itasaidia kupembua jambo hilo kwa kina na kutafakari njia au hatua sahihi za kukabiliana nalo. Maelezo haya yanathibitisha kauli ya wahenga isemayo *haraka haraka haina baraka*. Hivyo, kuwa na subira pasipo kufanya papara kuna manufaa katika kuliendea jambo linalokusudiwa. Maarifa haya huandikwa kwenye vazi la kanga ili kusaidia jamii kukumbuka kwamba subira ni muhimu katika kutenda au kuamua jambo fulani.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili kuhusu namna vipengele vya epistemolojia ya Waafrika vinavyobainika katika vazi la kanga za Waswahili. Matokeo yameonesha kuwa kanga hizo zimeandikwa semi mbalimbali kama vile methali, mafumbo na misemo, ambazo huhifadhi maarifa ya kiepistemolojia yanayosawiri kaida zao. Maarifa yaliyobainika na kujadiliwa katika makala haya ni kuhusu: kuwepo kwa kani kuu ambapo kwao, Mungu anaaminiwa kwamba ni kiini cha asili ya kuwapo kwao ulimwenguni. Vilevile, Mungu anaaminiwa kwamba ni mfanikishaji na sababu mojawapo ya hatima ya mwanadamu. Pia, imani ya Waswahili imekitwa katika misingi ya kuthamini na kuheshimu kazi kama nguzo ya kustawi kwao kuanzia ngazi ya familia hadi taifa. Maishani mwao husisitiza jamii kufanya kazi kupitia sanaa yao, ikiwemo fasihi. Heshima na utiifu pamoja na uvumilivu ni masuala pia yanayozingatiwa na kuthaminiwa katika jamii ya Waswahili. Maarifa yaliyobainika kupitia semi zilizoandikwa kwenye vazi la kanga hudhihirisha mitazamo na tajriba za Waswahili kama jamii mojawapo inayopatikana barani Afrika.

## Marejeleo

Agozino, B. (2018). The African Philosophy of Forgiveness and Abrahamic Traditions of Vengeance. *ARAS*, 39(2), 239-252.

Aju, O. Et al. (2013). The Meaning of Work from the Nigerian Pespective. *European Jounal of Business and Managment*, 5(22), 154-162. https://www.researchgate.net/publication/282287583_

BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili ya BAKITA*. Longhom Publishers.

BBC News, (2017). Nguvu ya Vazi la Khanga Afrika Mashariki. https://www.bbc.com/swahili/habari-39459801

Beck, R. (2001). Ambigous Signs: The Role of Kanga as a medium of Communication. *Swahili Forum*, 68(1), 1-11.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu)*. Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Coser, L. (1963). *Sociology through Literature: An Introductory Reader*. Prentice-Hall.

Duwe, M. (2022). *Uchimuzi wa Eskatolojia ya Waafrika katika Mbolezi za Wangoni (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu)*. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Effingham. N. (2013). *An Introduction to Ontology*. Polity Press.

Etta, E. E. (2019). The Reality of African Epistemology. *Internatinal Jounarnal of Innovative Science, Enginnering and Technology*, 6(10), 279- 305.

Hanby, J., na Bygott, D. (1984). *101 Uses of Kangas: Fashionable, or Fanciful*. Jeannette Hanby and David Bygott Printers.

Kijogoo, S. D. (2021). *Saikolojia na Maisha: Ishinde Hofu, Boresha Maisha yako, Chagua Marafiki, Tunza Muda*. King Kijogoo Publishers.

Kisombo, C. I. (2022). *Lugha na Ujenzi wa Dhamira ya Maadili Mema katika Semi Zilizoandikwa kwenye Vazi la Kanga (Tasnifu ya Umahiri)*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Age. International Publishers.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia, na Misingi ya Uchambuzi*. Mture Educational Publishers Limited.

Mulokozi, M. M. (2017). Utangulizi wa Fasihi *ya Kiswahili*. KAUTTU Limited.

Murphy, G. L. (2003). *African - American Faith in America*. Oxford University Press.

Narizvi, S. (1982). *The Sociology of Literature of Politics*. Edamund Burke.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. DUP

Oladipo, O. (2004). Religion in African Culture: Some Concept Issues. *A Companion to African Philosophy*, 1(1), 355-365.

Oruka, H. O. (1990). *Trends in Contemporary African Philosophy*. Shirikon Publishers.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.